

REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Tuesday, 26th July, 2016

The House met at the County Assembly Chamber, Malindi Town, at 9.00 a.m.

[The Temporary Speaker (Hon. Ms. Ngala) in the Chair]

PRAYERS

QUORUM CALL AT COMMENCEMENT OF SITTING

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Mr. Clerk, is there quorum?

Clerk –at- the Table: No, we do not have quorum madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Ring the Bell.

(The Quorum Bell was rung)

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Okay, Mr. Clerk do we have quorum?

Clerk –at- the Table: Yes, we have quorum madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Next Order?

MOTION

**ADOPTION OF THE REPORT ON STALLED PROJECTS FOR THE DEPARTMENT OF
AGRICULTURE, LIVESTOCK DEVELOPMENT AND FISHERIES**

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Yes, Chairperson Agriculture, Livestock and Fisheries. Is he around?

Hon. Chai: Thank you Madam Speaker, for granting me the opportunity to stand in for the Chairperson of Agriculture to move the Motion:-

THAT, this hon. Assembly adopts the Report of the Sectoral Committee on Agriculture, Livestock Development and Fisheries on the stalled projects for the County Department of Agriculture, Livestock Development and Fisheries laid on the Table of this House on Tuesday, 5th July, 2016. I would like to call upon hon. Muhambi to second.

(Hon. Muhambi stood at his place to second)

(Question proposed)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Muhambi: Asante sana Madam Spika kwa kunipatia nafasi hii. Nami nimesimama kuunga mkono Ripoti hii. Nafikiri hii Ripoti iko na kila mmoja wa waheshimiwa. Madam Spika, Kamati ya Kilimo ilienda kutembelea hii miradi ambayo mingine kufikia ule wakati tukiitembelea, ilikuwa bado haijakamilika. Kwa kweli, Madam Spika, yale yote ambayo tumeyaona katika miradi hii ni kama vile ambavyo iko kwa hii Ripoti na baadhi ya yale mambo ambayo tumeyaona ni kwamba tulipofika eneo la Zowerani ambalo ni Wadi ya Tezo tulipata kwamba ule mradi ulikuwa umeanza lakini haujakamilika na sababu zilizofanya mradi huu usikamilike ni kwamba hakukuwa na maelewano baina ya wanakijiji na yule aliyekuwa amepewa hiyo kazi. Kitu kingine tulichopata hapo ni kwamba umeme ulikuwa bado haujawekwa kwa sababu yule mwanakadarasi alikuwa analalamika kwamba zile pesa zilizotengwa kutengeneza huu mradi hazikuwa zimewekwa katika ile bajeti.

Jambo lingine ni kwamba wananchi walikuwa wanalalamika wakidai kwamba hawakuhusishwa na kamati ilikuwa ikifanya mambo bila ya kuhusisha wananchi. Tulipofika Mtondia pale palikuwa na *Ukulima Bora Dairy Cooperative Society cooler* ambayo pia hiyo tulipata...Mwanzo hapa Mtondio tulipata kwamba kulikuwa na mradi uliokuwa umejengwa wakati wa mabaraza na huu mradi ulikuwa umejengwa katika uwanja wa Chifu. Halafu kukatokea mfadhili akajenga mradi mwingine wa maziwa na ule uliojengwa mwanzo ulikuwa unatumika na mambo mengine.

Wananchi walikuwa wanalalamika kwamba ile bei ambayo walikuwa wananunuliwa maziwa iko chini. Wakapendekeza mikakati ifanywe ili hiyo bei iongezeke. Tulipoenda Matsangoni tulipata kwamba mradi wa eneo hilo ulikuwa umesimama na bado haujakamilika kwa sababu ili kamati ambayo ilikuwa imewekwa kusimamia huo mradi haikuwa na maelewano mazuri na wananchi. Mambo yote waliyokuwa wakifanya hawakuhusisha wananchi. Kwa hayo nimesimama kuunga mkono Ripoti hii.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Asante. Any other contributions? Hon. Mwayaa.

Hon. Mwayaa: Asante sana mheshimiwa Spika...

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Excuse me, hon. Mlanda do you have an intervention to make?

Hon. Mlanda: Thank you Madam Speaker. We noticed some differences in our gadget here because all the lights are on, so we thought maybe the time we want you to pay attention on us you may not get our...but I see it is also working, as long as the honourable Member is on his...let me give him time. I did it before you gave him the permission to speak. So let me sit Madam Speaker.

Hon. Mwayaa: Asante. Hali ya mitambo mara nyengine huwa namna hiyo lakini kwa sababu tunawasiliana tutaendelea na kazi zetu za Bunge. Nasimama kuunga mkono Ripoti hii ya mambo ya Kilimo. Kusema kweli kitu chochote ambacho kinahusu kilimo mimi Mheshimiwa wa Kayafungo nakiunga mkono. Hili baa la njaa ambalo linaendelea na ikiwa miradi iliyoandikwa katika Ripoti hii itakamilika na iwe iliundwa kwa dhamira ya kupeleka mbele Kilifi yetu ama kwa ajili ya kilimo ambacho ni uti wa mgogo hasa katika kaunti yetu basi nitaunga mkono ili miradi yote imalizwe na tupige hatua mbele.

Baa la njaa linaloendelea Ganze na kwingine hata Kayafungo, tukizingatia ile miradi ambayo ilikuwa ni isaidie watu wetu wa Kilifi nafikiri lazima tuwe na mahali pa kuanzia. Wacha Ripoti hii ipite ili tuone tumesaidia vipi Jimbo letu la Kilifi na ile miradi ya kilimo tunayodhamiria kuifanya tuifanye ili tueleke mambo mengine na tusonge mbele upande wa

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

kilimo katika Jimbo letu la Kilifi. Naunga mkono miradi hii imalizwe na tusikomee pale tuanze miradi mingine ambayo itakuwa inasaidia watu wetu wa Kilifi.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Asante mheshimiwa.

Hon. Mlanda: Thank you Madam Speaker. I stand in support of the adoption of this Report on Agriculture and urge the Chairperson that we should come up with modalities to get rid of the hunger in our county. It is so sad that we have projects which are still stalled and we do not know how long these projects will take to be finalized so as to make sure that, the people are enjoying the fruits of devolution in Kilifi County.

Agriculture is the backbone of any country and it looks like most of us have ignored agriculture and embarked on some other activities. If we could have done this before... we had one of the investors from Netherlands; he gave us some advice on how we can uplift our standards on the side of agriculture, livestock and fisheries but all this went to the dust bin. I call upon the Chairperson and his Committee to again come up... so that we can avoid this hunger that is biting in Ganze and some other areas of Kilifi County. I stand to support the adoption of this Report. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. Mlanda. Hon. (Ms.) Chiku.

Hon. (Ms.) Chiku: Thank you Madam Speaker. I was about to say Sir. I rise to support this Motion on the adoption of the Agriculture Report. As a Member of the Committee on Agriculture, I had a chance to go round in Tezo Ward but I was committed and was not able to go round the other places. I want to put a say on the Zowerani cooling station which has stalled due to funds. It was budgeted for Ksh.5 million, and the people of Tezo were up in arms why this project is not completed.

I got very disturbed and I did not know how to start until the hon. Speaker Mr. Jimmy Kahindi came up with a suggestion that we should do oversight on several Committees and I was very happy about it. I got a chance to go to Zowerani and it was shocking; the contractor had absconded and the materials were put in the chief's office and they were being vandalized. We did not manage to get the Chairperson of the Zowerani committee but the area senior chief briefed us on what was happening. The committee took it up and we called the CEC (Chief Executive Committee Member) of Agriculture and he gave us flimsy reasons on the stalemate of this good project.

I am happy to report after that oversight and after calling the CEC here that Zowerani cooling station is almost completed and I am sure it will be handed over to the farmers who were up in arms, I must say. I met Mr. Mangi who is the chairperson several times who told me he had made several visits to the CEC's office. Also, while we were still in Tezo Ward we managed to visit the cattle dips. They were in shambles and the amount to which they had been paid for was exorbitant; for example, the cattle dip in Tezo was awarded Ksh.2 million and they used very cheap material in the matter of two iron sheets to cover the dip.

While the CEC managed to explain the situation we agreed that we have to see that it is completed because there is another cattle dip in Kilifi South which was very badly made and in fact the Chairperson of the Agriculture Committee hon. Gambo told us if an animal would have gone in that cattle dip it would not have come out alive. We were shocked about these projects which were going on.

Anyway we managed to arrest the situation in my area Tezo but there is another sad thing Madam Speaker about Fisheries. Hon. Mlanda spoke about it and I also think we should put some effort on it. By now, Kilifi County as it is, is suffering from hunger; we should be

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

practicing irrigation because the business of farming during the rainy season is something of the past. Other areas are actually using mechanized agriculture.

I would also like to say something about fishing. As you know Madam Speaker, Kilifi beach is the widest compared to Kwale and Mombasa and there was some interest of a fishing port at Gongoni. I do not know how it was watered down but also I would like to point out in this House that the yellow tuna which is very expensive and nutritious and it is a very good product in the world, comes from Kilifi. We have poachers coming in to poach the fish and process our fish in their countries like Seychelles and that product is sold as meat while it is actually the yellow tuna. We had big ideas about fishing factory at Gongoni where we were going to use the waste as fertilizer; we would have recycled the waste from the fish.

We also managed to speak to fishermen about their BMUs (Beach Management Units); there were fishing boats which were distributed to Mnarani but other areas are still waiting and it is taking long. We do not know why it is taking long for these fishing boats to be distributed to the other areas. There is also a myth over icing factory. Fishermen are complaining but we will tackle this in the next Agriculture Committee. Thank you very much for giving me this time.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. (Ms.) Wanje Chiku. Hon. (Ms.) Jane Bahati Mwaro.

Hon. (Ms.) Mwaro: Asante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Mimi nami naomba niweze kuchangia nikiwa naunga mkono Ripoti hii ya Kilimo ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, ni bayana kwamba baadhi ya sehemu za Kaunti ya Kilifi zimekumbwa na njaa. Nikizungumzia kwa muktadha, juma lililopita siku ya Ijumaa tulikuwa kule Ganze sehemu hasa inaitwa Ngamani kwa ajili ya kugawa chakula cha msaada. Tukaenda mpaka sehemu moja inaitwa Mrima wa Mlungu kugawanya chakula cha msaada. Nikiangalia Ripoti hii ninayo machache ya kuzungumzia maana mimi sio Mwanakamati lakini nakala hii niliipata kwa muda ufaao na nimeweza kuiangalia kwa kina.

Mheshimiwa Spika, tunakuta kwamba kuna hii miradi ambayo iko katika sehemu tofauti katika Kaunti ya Kilifi. Tukiangalia hasa Zowerani kuna ule mradi ambao haukukamilika na sababu ambazo zimefanya mpaka mradi ule haukukamilika ni kuwa kulikuwa na malumbano kati ya wale watu ambao wanaishi pale. Lile ambalo naweza kuongea ni kwamba wakati hii miradi inaanziwa katika sehemu hizi, tunajua hii miradi iliwekwa kule ikiwa na sababu ambayo ni kwa ajili ya kusaidia wananchi wa Kilifi. Hivyo basi, hii iliwekwa kule ikiwa na sababu na ikiwa inakwama basi miradi hii unakuta kwamba haitaweza kuwafaidi wananchi wa Kilifi. Ningependa kusema kwamba mahali popote ambapo pana malumbano yakaweze kusitishwa ili tuweze kuona miradi hii imefikia kikomo na wananchi pia waweze kunufaika.

Mheshimiwa Spika, kuna mradi mwengine upande wa Matsangoni; wanakamati walipoenda kule walikuta mradi umesitishwa kwa sababu pesa zilikosa kutayarishwa kwa wakati unaofaa. Wanakandarasi walikosa pesa zao ndipo mradi ule ukasitishwa. Ningependa miradi hii iweze kuzingatiwa ili kama imekwama kwa ajili ya pesa, pesa zinapopatikana hii miradi iweze kukamilika ili hizi sehemu zipate kufaidika na hii miradi. Maana miradi hii ni muhimu na watu wana sababu... maana hii miradi haikuwekwa tu bali ni wananchi walioulizwa na wakaweza kuidhinisha kwamba kuna umuhimu na miradi ile.

Ombi langu ni kwamba wakati wowote mradi wa serikali unapowekwa mahali tuone kwamba pande zote zinazohusika, upande wa *Executive* na upande wa Bunge zile sehemu ambazo zinahusika na miradi hii, wacha miradi hii ikafanyike kwa wakati ufaao ili tuone yule mwananchi naye ameweza kunufaika. Mheshimiwa Spika naunga mkono na naomba kwa ruhusa yako nikaweze kuketi. Asante.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon. (Ms.) Jane Mwaro. Hon. Fondo.

Hon. Fondo: Asante sana Madam Spika. Mimi nami naunga mkono Ripoti hii tuweze kuipitisha. Nikiwa si mmoja wa wale wanakamti wa Kilimo lakini Ripoti hii nilipoipata niliangalia mengi sana; niliangalia zile picha za ile mijengo kwa sababu ya miradi ya ukulima. Sasa kuunga mkono kwangu mheshimiwa Spika ni kwamba mapendekezo yale ambayo yamependekezwa na kamati hii ni mazuri sana kwa sababu wakati kama kuna miradi, kandarasi kama zinapeanwa ile kamati husika ambayo inapeana kandarasi izingatie nani ambaye anaweza kuchukua mradi huu na kuumaliza kwa wakati unaotakikana.

Wananchi wana matarajio mengi sana; kwa mfano, katika mradi wa Zowerani wananchi wenyewe walipendekeza ya kwamba mradi ule uwe pale ili uwafaidi kwa yale yote ambayo yanatakikana. Kuna manufaa ambayo walikuwa wapate kulingana na huo mradi lakini sasa inaonekana ya kwamba wale ambao wanapewa hizi kandarasi ndio ambao wengine hawana fedha za kujenga ama kumaliza ule mradi kwa wakati unaofaa. Haya mapendekezo ya kamati ambayo wameyaweza hapa sitayasoma kwa sababu kila Mbunge katika Bunge hili yuko nayo. Haya yote yakiwa yanaweza kuzingatiwa basi mambo kama haya hayataweza tena kutokea kwa wakati unaotakikana.

Yangu ni kuunga mkono hayo yote ambayo yamewekwa hapa. Tunajua vyema ya kwamba katika Kaunti ya Kilifi, ukulima ni uti wa mgongo na kaunti yetu kumeingia njaa na mambo kama haya ndio ambayo sisi kama Bunge tunaweza kuzingatia. Vile vile wale ambao wamekuja na mwito wa kwamba wakasaidie watu wa kule Ganze, tumeona kwa runinga ya kwamba Bunge hili limepeana chakula kwa sehemu fulani fulani. Haya yote yanaletwa na ukosefu wa mvua.

Kwa hivyo yale yote ambayo yamenakiliwa na kamati hii tuweze kuyapitisha ili kwamba isiweze tena kujiregelea. Wale ambao wanaweza kupewa kandarasi wamalize wakati unaofaa. Naunga mkono haya yote ambayo yamenakiliwa hapa Mheshimiwa Spika. Asante sana.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Asante mheshimiwa Fondo. Mheshimiwa Zawadi.

Hon. (Ms.) Zawadi: Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi nami nasimama kuunga mkono Ripoti hii ijapokuwa si mwanakamati wa Kilimo. Yale yote yaliyoangaziwa na kamati hii kusema kweli, wameangazia mambo muhimu sana kwa sababu tukiangalia sisi kama viongozi wa Kilifi ile hali ambayo inaendelea hapa Kaunti ya Kilifi sio ya kufurahisha. Kuna Wadi nyingine hivi tunavyoongea ni walalahoi kwa sababu ya njaa wanayoipitia.

Mambo haya ya kilimo yanapozingatiwa kwa sababu kilimo ni uti wa mgongo na kilimo ndio kila kitu katika maisha ya mwanadamu... na hakuna yoyote atakayesimama na apinge Ripoti hii. Sisi kama Wabunge wa Kaunti ya Kilifi, juzi wafanyikazi wetu wa Bunge walitupatia changamoto nzuri sana. Walitoka hapa na wakaenda eneo la Ganze na hao ni wafanyikazi tu. Walijitolea kujiunga na wale ambao wameathiriwa na baa la njaa. Tukaona kwamba wafanyikazi wetu wa Bunge la Kilifi wako pamoja na sisi kama wabunge. Tunafanya kazi lakini wao wako pamoja na sisi wakiwa msitari wa mbele kuenda kulia na watu wa Ganze.

Sisi kama viongozi wa Kilifi tumesimama hapa kupongeza kamati ya Kilimo kwa kazi yao nzuri na mimi nimesimama kuunga mkono na kuwapa pongezi wale wafanyikazi wote wa Bunge la Kaunti ya Kilifi walioenda Ganze na kupeana msaada wa chakula. Asanteni.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Asante mheshimiwa Zawadi. Any other contributions? Yes Hon. (Ms.) Arafa

Hon. (Ms.) Arafa: Thank you very much Madam Speaker for giving me this opportunity to contribute to this Report on the adoption of the Report on Agriculture, Livestock and Fisheries. First, I want to congratulate the Committee on Agriculture, Livestock and Fisheries for the good work. I have gone through the Report and some of the projects I was looking to find out if they really visited these areas and I am happy that they have been captured in this Report.

I am happy that some of the hon. Members have stood here to really support and air out their views that people in Kilifi County are dying of hunger. Madam Speaker, to my understanding and also to the way I understand Kilifi County and some of the resources we have in this county, Kilifi people are not dying of hunger but poverty. The Committee on Agriculture here has found out some of the best activities and projects that if fully implemented, we can curb the issues of hunger and poverty in Kilifi County.

Madam Speaker, why am I saying this? There are other projects that even if we try to do them in Ganze or in other parts of this county without surveys or without proper information on the same, we will stand here and say Ganze people are dying of hunger. It is not a must that we do Agriculture in Ganze; there are other viable projects that if taken to Ganze can do well. We have to sit as leaders and as one team. The Committee of Agriculture, I know there are very good experts and professionals in Kilifi County who can deliver and give us very good information on Agriculture and on what are the best activities to be done in Ganze.

A good example is when we passed in this House the issues of solar harvesting and wind energy; they are dying of hunger because there is no rain. If there is no rain, can we have water for irrigation in Ganze? Some of these things we have to find what are the some of the best activities we can do to our Kilifians.

Another thing I want to contribute on is the issue of the cooling system that we have in Kilifi County. If there are no rains but we are privileged to have the wide and open sea and I am happy hon. (Ms.) Asha Chiku Wanje talked about the yellow tuna; there are a lot of people benefiting in Kilifi County. There are tonnes and tonnes of yellow tuna that are coming from Kilifi County and I am happy this House... there is a time we came up with the issue of a fish port in the county but even in this Report I have not seen any place that has been set aside for that.

On the issue of rain, it is an international disaster. It is an issue of climate change. Even if you want to plant maize we do not have rains and we do not have any ways of doing irrigation. I think the issue of fishing can do well in Kilifi County. It is very sad and pathetic to find some cooling systems that were introduced by the Department of Agriculture upto date most of the projects are still stalled. We have a very active fish deport in Uyombo and Watamu where a lot of people from Tanzania (the Wapembas) are there. If you want to eat fish go to Watamu or Uyombo and you will get as much fish as you want.

There are a lot of activities which if fully implemented and they have proper mechanisms, they can do very well. Zowerani is one of the areas in Kilifi County in Tezo Ward where they produce a lot of dairy products and when you go there try to drive to Kilifi in the morning and see the amount of plastic jerrycans people are rushing taking milk to Mombasa and yet we have a cooling system which has been staying there for years. I think hon. Members we have to prioritise when coming up with projects. Some of the projects if we had catered for them from our first year by this time we would not be talking of issues of hunger and drought in Kilifi County.

Another thing that I want to talk about is the short income generating activities. Yes, everyone is now talking about Ganze and Magarini but I am telling you even in Malindi some

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

people are dying of hunger. So, we have to find the kind of income generating activities which can do well in Kilifi County to make sure that everyone benefits from the resources we have and more so in agriculture. Everywhere people are working hard to make sure that they contribute as much as they can. There is very good business that everyone can do; if you open a restaurant, you will not miss a customer because everyone has to eat. So, we have to make sure that we have enough on our table before doing anything.

Another challenge that I would wish to point out from the Report is the BMUs. As a County, we are working very hard to make sure that the BMUs are doing very well but they have a lot of challenges on the ground. Some of the cooling systems are owned by very few individuals. Before these projects are completely owned, we should make sure that there are good structures on the ground before they start operating. Otherwise, they are going to be owned by only two or three individuals who feel that they are the key custodians for the fisher folk family. Thank you very much Madam Speaker. I again wish to congratulate the Committee on Agriculture for the good work done. Thank you.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Thank you hon...Hon. Kambi please.

Hon. Kambi: Asante sana Madam Spika. Mimi pia nasimama kuunga mkono Ripoti hii. Wacha nipeane pongezi kwa Kamati hii kwa ukakamavu waliofanya kuweza kuona miradi ile ambayo imesimama iweze kurekebishwa na mikakati ambayo imewekwa katika Ripoti hii ili miradi yetu ikamilike na kunufaisha wananchi wetu katika Kaunti ya Kilifi.

Madam Spika, jambo hili la njaa katika Wizara ya Kilimo ni jambo la kuhuzunisha. Sababu kubwa imeletwa na serikali kuu. Tukiangalia katiba ilivyonena, kila jukumu lilipatiwa serikali yake. Kuna majukumu ambayo yalipatiwa serikalali zetu za kaunti lakini ni jambo la kusikitisha kuona kwamba pesa zote, karibu robo tatu zinabaki katika serikali kuu ambayo pesa hizo zinastahili kumilikiwa na serikali zetu za Kaunti. Ndio sababu unaona miradi mingi sana upande wa kilimo haiwezi kukamilika kwa wakati unaofaa kwa sababu wakati mwingine pesa huwa hazitoshi. Ukiangalia karibu pembejeo zote za Kilifi robo tatu ya matinga yamelala na ukiuliza unaambiwa ni mambo ya pesa. Ukiangalia pesa zote robo tatu zimetengewa serikali kuu. Ni jambo la kusikitisha kuona ya kwamba serikali hii ambayo inaongozwa na Uhuru Kenyatta na Ruto...

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

Hon. Mramba: Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Hoja ya nidhamu nikiomba mheshimiwa wa Marafa anayeongea hivi sasa, amesema kwamba robo tatu ya yale matinga yalinyonunuliwa na Kaunti yamelala. Anaweza kututhibitishia kwa sababu matinga yale yamenunuliwa kwa pesa nyingi? Hivyo basi kama yalinunuliwa matinga ambayo ni gushi, tuweze kujua kwenye Bunge hili. Asante.

Hon. Kambi: Mheshimiwa Spika, nataka kumjibu mheshimiwa...

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Another point of Order from hon. Stephen Mlanda.

Hon. Mlanda: Asante sana mheshimiwa Spika. Namuomba mheshimiwa mwenzangu ambaye analalamika kuhusu serikali kuu ya kwamba janga hili linasababishwa na serikali kuu... Sasa ikiwa ameangazia ya kuwa pesa haziji na ndio sababu ya kwamba shida hizi tunazipata katika serikali yetu ya Kaunti ya Kilifi, je, haya mambo ya matingatinga pia yanasababishwa na serikali kuu kwamba inafanya matingatinga haya yasifanye kazi?

Hon. Kambi: Mheshimiwa Spika, nataka kumjibu mheshimiwa wa Kakuyuni. Nafikiri pengine nilipokuwa naongea hakuwa makini sana; labda alikuwa anafwata shughuli nyingine

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

lakini mimi sikuongea mambo kama hayo aliyokuwa anaongea. Mheshimiwa Mlanda, nafikiri utakubaliana na mimi ya kwamba Sekta ya Kilimo katika Katiba yetu imegatuliwa na ukiangalia pesa nyingi sana zinabaki upande wa serikali kuu. Hali hii imeleta shida kwa sababu pesa zikija kidogo utakuta hata wakati ambao pengine ni tinga zetu ziende kurekebishwa haviwezekani kwa sababu pesa zimekuja kidogo na hiyo ndio sababu ambayo tumepata shida. Tukiangalia kilimo ndio uti wa mgongo na kama hauwezi kuangaziwa...

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): There is a point of intervention.

Hon. (Ms.) Muthoka: Asante mheshimiwa Spika. Nataka tu nimfahamisha mheshimiwa aliyesimama ya kwamba serikali kuu haina uhusiano wowote na janga la njaa ambalo liko katika Kaunti ya Kilifi. Upungufu wa pesa za Sekta ya Kilimo sio Kaunti ya Kilifi peke yake na maeneo mengine hatujaona yakikumbwa na njaa kama Kaunti ya Kilifi. Ni wakati wetu wananchi wa Kaunti ya Kilifi tuje na njia mwafaka za kuboresha kilimo lakini tusirushie lawama serikali kuu. Tafadhali.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Another intervention.

Hon. Mlanda: Asante sana mheshimiwa Spika. Nafikiri mheshimiwa hatupatii taarifa ya kisawa kwenye kikao hiki. Angelituelezea ile shida hasa ambayo inafanya matingatinga haya hayafanyi kazi kwa sababu hatuwezi kupewa pesa tununue matingatinga ishirini halafu tupewe pesa za kutengezea matingatinga yale. Mbali na kuwa matingatinga yale kwamba hayafanyi kazi, tumekuwa na shida pia ya kuwa matingatinga yale hayana mafuta. Katika wakati huu wa kilimo tulikuwa tunahitaji matingatinga haya yalimie wananchi na ikasemekana kuwa matingatinga yale hayana mafuta. Je, ukosefu wa mafuta pia nao ni serikali kuu?

Hon. Kambi: Mheshimiwa Spika, ningependa kidogo waheshimiwa ambao wanauliza swala hilo waweze kuwa makini kama ninaongea. Sekta ya Kilimo iligatulia kikamilifu. Ni sababu gani inafanya serikali kuu kubaki na zile robo tatu za pesa? Kama zingechiliwa, tungekuwa na shida? Inastahili ziachiliwe basi tulalamike kwamba kwa nini kuna hivi na hivi? Tunalalamikia mambo ya pesa kwa sababu kama ni mambo ya ujenzi hakuna haja ya kupanga. Waziri wa Kilimo katika serikali kuu ikiwa pesa zile zilitengwa ziweze kusimamia Kaunti...

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): We have a Point of Intervention from hon. Hamza.

Hon. Hamza: Asante sana mheshimiwa Spika. Ningependa sana hata mimi kumuona mheshimiwa akiendelea kuzungumza ijapokuwa naona kuna maswali mengi sana ambayo yanamjia lakini hii inakuja kwa sababu ya maelezo yake ambayo anayapeana katika Bunge hili ambayo hatuwezi kuyathibitisha. Akizungumzia kuhusu swala la huduma haswa katika upande wa Kilimo ziko na changamoto kwa sababu kuna robo tatu ambayo imezuiliwa katika serikali kuu. Ni vyema azungumze robo tatu hii anayozungumzia ni gani haswa? Tunajua kuna mgao wa kifedha ambao hauko katika robo tatu ambazo anazungumzia labda pengine kidogo hesabu ziwe zinaenda kado. Ninaomba mneneji aeleze kinagaubaga robo tatu anazozitungumzia ni zipi tafadhali?

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Yes hon. Fondo.

Hon. Fondo: Asante sana mheshimiwa Spika. Naona yule ambaye anazungumza saa hii ni kwamba yuko nje ya Mada. Wakati huu tunazungumzia kuhusu hii Ripoti ambayo kuna miradi haijamalizwa na sababu hizo haswa ni gani? Wakati Kamati ilipozunguka iliona nini? Sasa yale mapendekezo yake, je tumeyakubali ama hatujayakubali? Kwa hivyo sijui kwa nini anazungumzia mambo ambayo hayafanani na Mada ya hivi leo.

(Applause)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Kambi: Asante sana. Mimi niko kwa mada na nimesimama kwanza nikasema naunga mkono Ripoti hii. Ripoti hii ina upungufu wa pesa ambazo zinasababisha miradi mingine kukosa kuendelea. Miradi mingine inatengewa pesa ambazo hazitoshi. Haya yanatokea kwa sababu pesa hazikuachiliwa zote kama alivyoongea mheshimiwa Hamza. Kama tujuavyo tunapata asilimia 100 na asilimia robo ndio inagawanywa kwa Kaunti zote 47 kwa hivyo robo tatu ya pesa zinabaki kwa serikali kuu. Hiyo inadhihirisha wazi kwamba kile kiwango cha pesa katika sekta ya Kilimo kuna robo tatu zinabaki, mheshimiwa naomba hapo uelewe. Nasimama kuunga mkono Ripoti hii.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): Hon. Hamza.

Hon. Hamza: Thank you Madam Speaker. I think up to this moment the hon. Member who is on the Floor is misleading this House. I just wanted to know exactly which amount he is talking about. On the issue of three quarters, what is being shared to the counties is 15 percent and 15 percent does not in any way translate, whatever mathematics you do whether from Magarini or Kilifi North constituency does not reflect to three quarters. Therefore, I would like the hon. Member to withdraw because he is misinforming the House. It is 15 percent and not three quarters unless he can justify if he happens to have documents that can really justify that it is three quarters; as far as I know it is 15 percent. We want to know what kind of mathematics he is working on.

Hon. Kambi: Mheshimiwa Spika, katika asilimia 100 ukitoa asilimia 15 zikibaki 85, robo tatu ni ipi? Ni hii 85 ama 15? Kama mheshimiwa anavyouliza kwa sababu tunavyojua katika 100 ukitoa 15, 85 ndio robo tatu, sasa sijui kama pengine hesabu anayoongea ni Ipi?

Hon. (Ms.) Sophie: Asante sana mheshimiwa Spika. Mimi naunga mkono Ripoti hii...

Hon. Mramba: Mheshimiwa Spika ninavyoona Hoja ya mheshimiwa wa Marafa asilimia 15 kwa 85, asilimia 15 haziwezi kuingiliana kwa robo tatu na ukweli ni kwamba ukifanya hesabu utaona asilimia 15 inaingia karibu mara sita kwa mia. Kwa hivyo zile hesabu alizozifanya kule Marafa haziingiliani tafadhali.

Hon. (Ms.) Sophie: Asante sana mheshimiwa Spika. Nataka kuwashukuru sana wanakamati wa Kilimo na Mwenyekiti wao. Mimi pia naunga mkono Ripoti hii. Nikikumbuka sisi wabunge ni wawakilishi wa wananchi. Ripoti hii imezungumzia mambo ya umuhimu kuhusu kilimo. Kuna mambo mengi yalikuwa na utata lakini wanakamati wameingilia kati na ninashukuru kwamba miradi kama hii kwa hakika sisi tukiwa wasimamizi wa wananchi wetu kuna mambo mengi katika Kaunti ya Kilifi yataendelea vizuri. Sitaongea mengi ila kuwapongeza na pia kuhimiza Kamati nyingine ziwe tayari kusimama kwa ajili ya wananchi wetu. Hili janga ambalo linazungumzwa kuhusu mambo ya njaa sio njaa bali ni umaskini kama vile mheshimiwa Arafa alivyosema. Kusema kweli, wengi wetu hatuna ufahamu kuhusu mambo ya kilimo. Naunga mkono na kusema Ripoti hii ipitishwe na tuendeleo na kazi zetu.

(Question, that the Mover be now called upon to reply, put and agreed to)

Hon. Chai: Thank you Madam Speaker for giving me some time to stand and congratulate the hon. Members who stood up in support of the Report and I was very happy that they were jubilant in support and were arguing very actively which is very nice for Kilifi County. My submissions will be short; I am standing in for the Chairperson of Agriculture today...

(Hon. Chai's microphone went off)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Thank you Madam Speaker. I was going through the recommendations of the Committee and I would like us to go through them. Allow me to read them so that they get into the hon. Members minds:-

“That, the Department should ensure that tenders are awarded to contactors who have financial capacity to ensure that projects do not have to wait for disbursement of funds from the County Government before they start to work.

Secondly, the Chief Executive Committee Member should ensure that the length of time required to release funds needed for the project is considered during the project pre-planning stages before determining or agreeing on projects status to ensure on time project funding.

Three, the Department should put measures to ensure that those contractors who do shoddy jobs are never awarded any contracts in future.

There is a need to put more effort in capacity building farmers to ensure that facilities are put to full use by the beneficiaries.”

I think I will add something on number four where there is the need to put more effort in capacity building; this is for us hon. Members; we have a part to play. As most of the contributors said that they were not in the Committee but I think it is your duty as hon. Members to educate your people well before a project has come. When we went out we found out that some of the projects were opposed by the community hence making the projects to stall. The problem of stalled projects was not just because of money or the contractor but I think some of the projects were opposed by the community. So there is need to put more effort in that.

“Five, there is need for the Department to ensure that there is constant monitoring of the projects to help in correcting errors as early as they occur to avoid wastage of county resources. Six, the Department come up with measures to ensure that the community is involved in one way or the other to avoid alienating projects meant to benefit them.”

These are the recommendations we as a Committee on Agriculture, Livestock and Fisheries came up with. My opinion to what some of the hon. Members have contributed on poverty and hunger from some of the areas in our County, Madam Speaker, I would like to put some comments or advice on these areas. Some of these areas are productive enough but it is just because of our culture of planting maize and maize only. It is our duty as hon. Members to spell out and see that we bring our community from this culture of maize and maize only because most of the areas if you go, like in Bamba Ward or even parts of my Jaribuni ward, you will find that people are just planting maize only so if you miss maize you miss everything and that brings hunger or poverty.

In most of the farms, if we grow fruits then in case maize fails at least one can sell the fruits or eat them. We have short rains products which we can plant and most of the farmers are not putting into consideration these products and that is why you will find if maize fails then they have nothing to go to as a subsidiary. If we go down there and educate our people that if you plant maize you can even have some trees in the farm to protect the environment and even sometimes if you do not have maize you can cut these trees and sell them or you can have cassavas in these farms and it will be well. We will be solving the problem of hunger or poverty. With these few remarks, I stand to congratulate everybody who has contributed towards the Report and I thank you Madam Speaker and wish all the best to the Members. Thank you very much Madam Speaker.

The Temporary Speaker (Hon. (Ms.) Ngala): I now put the Question.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

(Question put and agreed to)

ADJOURNMENT

There being no other business, I move to adjourn this House until 2:30 p.m. today. Thank you.

The House rose at 10.47 a.m.